



Strengthen Agency for Social Accountability

FORUMCIV.

Power to change



Strengthening Enabling Mechanisms for Accountability

ADOT ina mradi mpya unaoitwa **SEMA** ambao unahusika na Kuimarishe mifumo ya uwajibikaji. Mradi huu unafadhiliwa na Forumciv kupitia mpango wake wa **SASA** yaani Wakala wa kuimarishe uwajibikaji kwa jamii.

LENGO LA SEMA

Kuimarishe utaratibu wezeshi wa uwajibikaji kwa kukuza utawala shirikishi na haki za binadamu, kwa kuzingatia haki za watu wenyе ulemavu.

MATOKEO YA SEMA

Kuimarishe uwajibikaji katika muundo wa uongozi wa serikali za mitaa katika kukabiliana na masuala ya makundi mbalimbali hususani watu wenyе ulemavu. Pia kuongeza na kuboresha mijadala yenyе kujenga kati ya wananchi na viongozi.

Malengo ya SASA yamekuza Malengo ya SEMA ambayo nayo yamekuza matokeo ya SEMA kupitia shughuli nane (8) ambazo zimegawanyika katika makundi makuu matatu (3) ambayo ni.

Kukuza uelewa kuhusu mambo yahusuyo utawala shirikishi na haki za binadamu kwa kuzingatia watu wenyе ulemavu katika ngazi za serikali za mtaa.

Kujenga uwezo kwa watu wanaosimamia haki za wenyе ulemavu na wabeba wajibu (viongozi wa mitaa) katika ngazi za mitaa kuhusu masuala ya haki na haki za watu wenyе ulemavu pamoja na uongozi shirikishi.

Kukuza na kuimarishe mijadala katika jamii kuhusu masuala ya utawala shirikishi na haki za watu wenyе ulemavu kwa kuzingatia ulemavu wao.

SEMA IMELENGA MAKUNDI YAFUATAYO;

- Mtu mwenye ulemavu**
- Watu wanaowahudumia watu wenyе ulemavu**
- Viongozi wa serikali za mitaa**
- Wanajamii**
- Vikundi vya kijamii**
- Wadau wanaojihusisha na Watu wenyе ulemavu**
- Mitandao ya mashirika ya kiraia (AZAKI)**



Kata ya Chamazi na Sandali,
Temeke, Dar Es Salaam-Tanzania